Dhambi Dhidi Ya Roho Mtakatifu

na

Ellis Forsman

Dhambi Dhidi Ya Roho Mtakatifu

na

Ellis Forsman

Oktoba 7, 2011

Dhambi Dhidi Ya Roho Mtakatifu

Dhambi isiyo samehewa

Math. 12:22-32

Kutokuelewa kumetanda kuhusu "*dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu"* wengi wamehitimisha kwamba hii ni *"dhambi isiyo samehewa"* wanaweza kuwajibika leo; vinginevyo mtu mwenye hatia hana tumaini ya wokovu.

Ni nini maana ya dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu?

Ni *"ni dhambi isiyo samehewa"* ni lazima kuwe na jibu katika maandiko Matakatifu.

Kitabu kikubwa cha Concordance:

Kukufuru: 0988 blasphemia {blas-fay-me'-ah} kutoka katika 989 Kashifu, kuharibu, matamshi ya kuharibu jina zuri la mtu mwingine. Matamshi ya kuharibu inayogawanya kishujaa. KJV: kukufuru 16, kitalu 2, mazungumzo mabaya

Kamusi ya Vine ya maneno ya Agano la Kale na Jipya:

Kukufuru: tokana na blapto, kujeruhi, na *furu,* tamko. Matamshi ya aibu, mazungumzo mabaya. Pia imetafsiriwa kama: *kashfa*.

Roho Mtakatifu ni mtu. Kukufuru Roho Mtakatifu ilikuwa ni wa kimataifa, dhihaka chafu dhidi Yake. Kuna tukio moja la wazi ambalo limeandikwa kwenye Biblia ambayo kiukweli inawezakusemwa kuwa ni *"Dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu"*. Hii inapatikana katika Math. 12:22-32:

Math. 12:22-32,*"Wakati ule akaletewa mtu mwenye pepo, kipofu, naye ni bubu, akamponya, hata Yule bubu akanena na kuona. Makutano wote wakashangaa, wakasema Huyu ndiye mwana wa Daudi? Lakini mafarisayo walipo sikia, walisema, Huyu hatoi peop ila kwa Beelzebuli mkuu wa pepo. Basi Yesu akijua mawazo yao, akawaambia Kila ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, hufanyika ukiwa, tena mji au nyumba yoyote, ikifitinika juu ya nafsi yake, haitasimama. Na Shetani akimtoa Shetani, amefitinika juu ya nafsi yake, basi ufalme wake utasimamaje? Na mimi nikitoa pepo kwa Beelzebuli, je, wana wenu huwatoa kwa nani? Kwa sababu hiyo hao ndiyo watakao wahukumu. Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. Ama awezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu ya kuviteka*

vyombo vyake, asipomfunga kwanza Yule mwenye nguvu? Ndipo atakapoiteka nyumba yake. Mtu asiye pamoja name yu kinyume change; na mtu asiyekusanya pamoja name hutapanya. Kwa sababu hiyo nawambia, kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho hawata samehewa. Naye mtu yeyote atakaye nena neno juu ya Mwana wa Adamu atasamehewa, bali yeye atakaye nena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao."

Kufuru dhidi ya Roho Mtakatifu

Hakuna shaka juu ya hilo. Yesu aliweka wazi kuwa watu hawa wali tenda dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu kwa kukufuru dhidi Yake.

Yesu alifanya muujiza mkuu na watu wakashangaa na kusema, "*huyu siyo mwana wa Daudi?"* lakini mafarisayo wakasema, *"Mtu huyu hatowi pepo, bali kwa Beelzebuli mkuu wa pepo."*

Yesu akajibu kuwa Anatoa pepo, siyo kwa Beelzebuli, bali kwa, *Roho wa Mungu".* Roho Mtakatifu alifanya kazi hii kupitia Kristo.

Mafarisayo walimkufuru Yesu kwa kutumia mkuu wa pepo kufanya miujiza; kwa hiyo, walikufuru (waliongea juu yake, wakatenda dhambi) Roho Mtakatifu, alifanya miujiza kupitia Kristo.

Walitambua kuwa miujiza ilifanyika kwa mkono wa Yesu, lakini walikataa kuhusika kwa Roho Mtakatifu kwa kusema Yesu alifanya miujiza hii kupiti Beelzebuli, mkuu wa mapepo.

Haiwezi kusamehewa

Kama matokeo ya dhambi ya kukufuru Roho Mtakatifu, Yesu akatangaza kuwa Mafarisayo hawa walitenda dhambi isiyo samehewa.

Math. 12:32, "*Naye mtu yeyote atakaye nena neno juu ya mwana wa Adamu atasamehewa, bali yeye atakaye nena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, hata ule ujao."*

Angalia kwamba Yesu alitangaza, *"...yeye atakaye nena neno juu ya Roho Mtakatifu, hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, hata ule ujao."*

- Kwanza, *"...hatasamehewa".*
- Pili, "*...katika ulimwengu wa sasa, hata ule ujao."*

Inamaanisha nini akisema *"hata ule ujao"?*

Msemo huu unamaanisha, kwamba kutakuwa na dhambi zitakazo samehewa *katika ulimwengu ujao?*

Tunatambua kuwa hakutakuwa na dhambi zitakazo samehewa katika umilele, ulimwengu ujao. Dhambi zinapaswa kusamehewa katika maisha haya, kama zinaweza kusamehewa.

Kristo alikuwa hazungumzii umilele Aliposema, "*hata katika ulimwengu ujao".*

Ulimwengu: kamusi ya Vine. Aion {ahee-ohn'} wakati, mda kitambo.

Toleo Jipya la Mfalme Yakobo inasema, "*Mtu yeyote akisema neno juu ya Mwana wa Adamu, atasamehewa, bali yeye atakaye nena neno juu ya Roho Mtakatifu, hatasamehewa, katika umwengu huu hata ule ujao."*

Hii inatoa mwanga zaidi.

Kiukweli, Yesu anawatangazia mafarisayo walio kufuru kwamba wametenda dhambi, au wamekufuru, dhidi ya Roho Mtakatifu aliye fanya miujiza hii kupitia kwake, na hawatasamehewa katika "*wakati"* (wakati wa Wayahudi), hata katika *"wakati"* ujao (Wakristo).

Yesu alifanya miujiza yake wakati wa Wayahudi; mitume walifanya miujiza yao wakati wa Wakristo. Dhambi hii haikuwa na msamaha.

Yesu alisema wangeamini kuwa ni mwana wa Mungu kwa kazi alizofanya.

Yoh. 10:36-38, "*je Yeye ambaye Baba alimtakasa, akamtuma ulimwenguni, ninyi mnamwambia, unakufuru; kwa sababu nalisema, Mimi ni mwana wa Mungu? Kama sizitendi kazi za Baba yangu, msiniamini; lakini nikizitenda ijapokuwa hamniamini mimi, ziaminini zile kazi, mpate kujua na kufahamu ya kuwa Baba yu ndani yangu, name ni ndani ya Baba."*

Je mwanadamu anaweza kutenda dhambi juu ya Roho Mtakatifu leo?

Watu wengi waaminifu wameongozwa kuamini kuwa mtu anaweza kuitendea dhambi Roho Mtakatifu leo, kwaku tenda dhambi isiyo samehewa dhidi ya Roho Mtakatifu, sawa na jinsi Mafarisayo walivyo fanya katika tukio hilo.

Lazima ikumbukwe kuwa Yesu alitangaza kuwa kunatofauti ya madhara ya kutenda dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu na dhidi ya Kristo.

Math. 12:32, *"Naye mtu yeyote atakayenena neno juu ya mwana wa Adamu, atasamehewa, bali yeye atakaye nena neno juu ya Roho*

Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao."

Yesu alipokuwa duniani, maneno aliyoongea yalikuwa yake, lakini miujiza aliyofanya yalifanywa na Roho Mtakatifu ndani yake.

Kulikuwa hakuna msamaha wa dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu, lakini dhambi zote dhidi ya Kristo zinaweza kusamehewa.

Ukweli swali ni hili, "binadamu leo hii wana tenda dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu, au dhidi ya Kristo?" Au tunaweza kusema, "dhambi ya mwanadamu leo hudaiwa dhidi ya Kristo au Roho Mtakatifu?"

Wengine wanaamini kuwa dhambi isiyo samehewa ni kutokuamini kuwa Biblia ni neno la Mungu na wengine hawaamini kuwa Yesu ni mwana wa Mungu. Kwa vyo vyote vile, kama dhambi hii ya kutokuamini ni dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu, je hiyo humaanisha kwamba mara mtu asiyeamini hawezi kubadilisha nia yake na kutubu? Paulo anasema mtu ana weza kubadilika. Chukuwa mfano ufuatao:

I Wakor. 7:12-16, "*Lakini watu wengine nawaambia mimi, wala si Bwana, kwamba iwapo ndugu mmoja ana mke asiyeamini, na mke huyo anakubali kukaa naye asimwache. Na mwanamke ambaye ana mume asiyeamini, na mume huyo anakubali kukaa naye asimuache mumewe. Kwa maana Yule mume asiyeamini hutakaswa katika mkewe, na yule mke asiyeamini hutakaswa katika mumewe, kama isinge kuwa hivyo watoto wenu wangekuwa si safi, bali sasa ni watakatifu. Lakini Yule asiyeamini akiondoka, na aondoke. Hapo huyo ndugu mume au ndugu mke hafungiki. Lakini Mungu ametuita katika amani. Kwa maana wajuaje wewe mwanamke kama utamwokoa mumeo? Au wajuaje wewe mwanamke kama utamwokoa mkeo?"*

Wawili wasioamini wana weza kutubu na kumkubali Yesu Kristo. Kutokuamini neno la Mungu au kutokuamini Yesu Kristo kuwa ni mwana wa Mungu siyo dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu.

Kufuru uliofanywa na Sauli (baadaye Paulo) ilikuwa dhidi ya Kristo, na siyo Roho Mtakatifu. Kabla ya kuongoka kwake, hakuamini kuwa Yesu Kristo ni mwana wa Mungu. Alisimama na kukubaliana na kusulubiwa kwa Yesu kwa sababu alikataa kuwa Yesu alikuwa Kristo, mwana wa Mungu. Hakuamini injil ya Kristo iliyo hubiriwa na Wakristo. Alikataa injili hii. Alilitesa kanisa kwa sababu ya kutokuamini kwake.

Na kama dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu ni kumkataa Kristo kuwa ni mwana wa Mungu au kukataa neno la Mungu kwa nini Mungu alimchagua kuwa mtume? Kwa nini Paulo aliruhusiwa hatakuwa Mkristo? Kama hii ilikuwa sababu, basi kwa nini kukufuru kwa Roho Mtakatifu hauku mtokea na Sauli? Sauli alikuwa mkufuru? Paulo anasema alikuwa, lakini haikuwa kufuru dhidi ya Roho Mtakatifu; ulikuwa ni ukufuru dhidi ya Kristo.

1 Tim.1:12-13, *"Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu kwa sababu aliona kuwa mwaminifu, akaniweka katika utumishi wake; ingawa hapo mwanzo nalikuwa mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri, lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani."*

Kutokuamini kwa Sauli na kupambana kwake hakukuwa dhidi ya Kristo na Roho Mtakatifu. Kufuru ilyofanywa na Mafarisayo katika somo letu lilikuwa dhidi ya Roho Mtakatifu walipoamini kuwa miujiza aliyofanya Yesu yalitimizwa na ibilisi na siyo Roho Mtakatifu.

Ukweli, Yesu alisema mateso ya Sauli ilikuwa dhidi yake. Matend. 8:3-5, *"Sauli akaliharibu kanisa, akiingia kila nyumba na kuwaburuta wanaume na wanawake na kuwatupa gezerezani. Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno. Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo."*

Kusudi kuu la miujiza ya Yesu Kristo na mitume lilikuwa ni kuonyesha kwamba Mungu alikuwa nao na mamlaka kuwa maneno waliyoongea yalitoka kwa Mungu. Ulikuwa ni uthibitisho kuwa Mungu alikuwa pamoja nao.

- Marko 16:20, "*Nao wale wakatoka, wakahubiri kote kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizo fuatana nalo,"*
- Waeb. 2:4, "*Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi,na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopewa mwenyewe."*

Yesu alimtuma Roho Mtakatifu awaongoze mitume katika kweli yote ambayo ilikuwa ni neno ambayo Yesu aliamuru Roho Mtakatifu kuwapa. Miujiza ambayo mitume walifanya ilitimizwa na Roho Mtakatifu ambaye alikaa ndani yao.

Yoh. 16:13-14, "*Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli atawaongoza awatie kwenye kweli yote, kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari."*

Ilikuwa ni dhambi isiyo samehewa mtu akidai kuwa Roho Mtakatifu hakusababisha miujiza. Miujiza hii ilikoma baada ya wakati wa mitume na wale waliyowekewa mikono na wao. Yesu alitoa kipawa cha Roho Mtakatifu "hadi" "umoja wa imani".

Waef. 4:7-13, "*Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo. Hivyo husema alipopaa juu aliteka mateka, akawapa wanadamu vipwa. Basi neno hilo alipaa, maana yake*

nini kama siyo kusema kwamba yeye naye alishuka mpaka pande zilizo chini ya nchi? Naye aliyeshuka ndiye yeye aliye paa juu sana kupita mbingu zote ili, avijaze vitu vyote. Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu. Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya uduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu,hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo."

"Umoja wa imani" ulikuwa umoja wa kipekee — imefunuliwa zaidi.

I Wakor. 13:9-10, "*Kwa maana tunafahamu kwa sehemu, na tunafanya kwa sehemu, lakini ijapo ile iliyo kamili,iliyo kwa sehemu itabatilika."*

Miujiza ambayo Roho Mtakatifu aliwapa ilikuhakikisha neno ilikoma wakati mitumu walipoweka pamoja neno la Mungu.

- I Wakor. 13:8,*"Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika, zikiwapo lugha zitakoma; yakiwako maarifa, yatabatilika."*
- I Wakor. 13:10, *"lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyokwa sehemu, itabatilika."*

Neno la Mungu lililo kamilika liliitwa sheria iliyo kamili ya umoja.

Yakobo 1:25, *"Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo,asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi huyo atakuwa heri katika kutenda kwake."*

Hatuna miujiza inayofanywa na Roho Mtakatifu leo. Ilikoma wakati wa mitume.

Haiwezekani kuokolewa?

Baadhi ya waalimu wa madhehebu wame tafsiri Waeb. 6:4-6 kama ushahidi kuwa mtu anaweza kufanya dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu leo na kuwa vigumu kuweza kusamehewa.

Waeb. 6:4-6, "*Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo, wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu, kwakuwa wamsulubisha mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi dhahiri."*

Haiwezekani: kamusi ya Strong, 102 adunatos {ad-oo'- nat-os} bila nguvu, dhaifu. Kwa maneno mengine, karibia inakuwa ngumu, lakini siyo kwamba haiweze kani jinsi tulivyo gundua neno.

Andiko hili halisemi kitu kuhusu "haiwezekani kusamehewa". Ugumu katika hili swala la upotofu ni kwa mtu hataki kutubu kwa sababu ya kugeukia pembeni kutoka kwa Mungu. Ni vigumu kwa mtu huyo kutubu.

Haisemi kwamba itakuwa vigumu kupata msamaha kama akitubu. Kifungu kwa uwazi inasema kwamba dhmbi ya mtu huyu ni dhidi ya Kristo, na siyo Roho Mtakatifu.

Waeb. 6:6, "*...kwa kuwa wamsulubisha mwana wa Mungu mara ya pili, kwa nafsi zao na kumfedhehi dhahiri."*

Yesu alisema katika Math. 12:32, kwamba dhambi yoyote dhidi yake itasamehewa. Math. 12:32, *"Naye mtu yeyote atakaye nena neno juu ya Mwana wa Adamu, atasamehewa, bali yeye atakaye nena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa, wala katika ule ujao."*

Dhambi au kukufuru dhidi ya Kristo inaweza kusamehewa. Dhambi ya Paulo dhidi ya kukufuru alisamehewa.

Dhambi inayotajwa katika Waeb. 6:6 ni dhidi ya Kristo, kwa hiyo, siyo dhambi isiyoweza kusamehewa.

Sura ya 6 ya Waeb haizungumzii dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu, dhambi hii ni dhidi ya Kristo, na siyo Roho Mtakatifu.

Hakuna dhabihu kwaajili ya dhambi

Imesemwa katika Waeb. 10:26 inazungumzia dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu, au dhambi isiyosamehewa.

Waeb. 10:26, "*maana, tukifanya dhambi makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi."*

Kifungu hiki hata hakiendani na "dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu".

Mtume analinganisha huiano kati ya sadaka ya dhambi chini ya Sheria ya Kale na sadaka moja ya dhambi chini ya sheria ya Agano Jipya, moja na sadaka ya kweli ya dhambi. Hakuna nyingine na haitakuwepo. Soma mazingira ya sura ya 10 yote ya kitabu cha Waebrania.

Mwana wa Mungu ni mmoja na sadaka pekee iliyo kamilifu!

Dhambi isiyo ya mauti

Dhambi dhidi ya Roho Mtakati diyo dhambi iliyotajwa katka I Yoh. 5:16-17, wakati mwingine inazungumziwa kama "dhambi isiyosamehewa?

I Yoh. 5:16-17, *"Mtu akimwona ndugu yake anatenda dhambi isiyo ya mauti, ataomba na Mungu atampa uzima kwa ajili ya hao watendao dhambi isiyo ya mauti. Iko dhambi ya mauti. Sisemi kwamba ataomba kwa ajili ya hiyo. Kila lisilo la haki ni dhambi, na dhambi iko isiyo ya mauti."*

Kutokana na kauli hii ni dhahiri kwamba mtu anaweza kuwa na hatia ya dhambi nyingi kiasi kwamba hata hakuna hitaji la kumwombea.

Hakuna udhibitisho, hatahivyo, kwamba hii ni dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu, jinsi Bwana wetu alivyoongea katika Math. 12:22-32.

Wengi wanarukia kauli ya Yohana "...*kuna dhambi ya mauti...*na wanadai dhambi hii (umoja) inamaanisha dhambi isiyo samehewa. Hataivyo, wanashindwa kuelewa kauli yake nyingine...*kuna dhambi* (umoja) *isiyo ya mauti..."*

Kuelewa kauli hii ni muhimu kuzingatia mazingira ambayo kifungu kimenukuliwa. Hebu na tuangalie cha 7 hadi cha 9 mistari ya I Yohana 1:

1 Yoh. 1:7-9, *"Bali tukitembea nuruni kama yeye alivyo wa nuruni, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Mwana wake, yatusafisha dhambi yote. Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."*

Mtume anathibitisha kuwa Kristo ni *"mwaminifu na wa haki kutusamehe dhambi zetu, na kutusafisha an udhalimu wote."*

Udhalimu wote unaweza kusafishwa!

Hali ya msamaha ya dhambi ya Mkristo inajumlisha toba, kukiri na sala. Kwa nyongeza juu ya kauli ya Yohana, ambao unahaidi msamaha wa Bwana kama tukikiri dhambi zetu, Yakobo akaongeza:

Yakobo 5:16, "*Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii."*

Kutoka katika maandiko haya tunaingizwa katika hitimisho kwamba Bwana atatusamehe dhambi zetu zote ambazo ndugu amezitubia. "*Dhambi isiyo ya mauti"* ni dhambi inayo samehewa.

Kama ndugu anahatia na dhambi Fulani na hatubu wala kukiri dhambi zake, hakuna haja ya Wakristo kumuombea ndugu huyo hadi atubu. Bwana hata samehe mtu huyo hadi atubu kiukweli.

Dhambi isiyo samehewa, au dhambi ambayo haisameheki?

Kuna baadhi katika ulimwengu wa madhehebu wanaoamini kwamba kukataa neno la Mungu au kumkataa Yesu Kristo kuwa ni mwana wa Mungu ni kufanya dhambi isiyo samehewa. Hiyo inaenda zaidi ya kile ambacho maandiko yanafundisha. Kuna wengine wanaosema kwamba husipoamini katika miujiza leo unafanya dhambi isiyosamehewa.

Lakini kama nilivyoonyesha hapo mwanzo, ishara za miujiza zimekoma wakati wa mwisho wa mitume.

Wale waliyokuwepo wakati wa mitume walishuhudia udhibitsho wa nguvu ya Roho Mtakatifu, nab ado tu waliikataa, walifanya dhambi isiyo samehewa. Hakuna njia nyingine wanayoweza kukubali nano la Mungu wanapo kataa uthibitisho wa Roho Mtakatifu uliyowaijia.

Tena hapa neno la Mungu:

Yoh. 10:36-38, "*Je Yeye Ambaye Baba alimtakasa, Ninyi mnamwambia unakufuru; kwa sababu nalisema Mimi ni Mwana wa Mungu? Kama sizitendi kazi za Baba yangu msiniamini; lakini nikizitenda ijapokuwa hamniamini mimi, ziaminini zile kazi; mpate kujua na kufahamu ya kuwa Baba yu ndani yangu, nami ndani ya Baba."*

Hatuna "uthibitisho" uliyooshwa leo katika hali ya miujiza.

Leo tunaamini hata kabla ya kuona miujiza.

Waeb. 11:1, "*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana."*

Biblia leo inatuambi kwamba tunaamini hata kabla hatuja samehewa.

Waeb 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao."*

Hadi tuamini kuwa Yesu Kristo ni mwana wa mungu hapo tunasamehewa. Mara tunapoamini na kutii neno lake hapo tunasamehewa. Kutokumuamini kristo ni dhambi dhidi ya Kristo, hainausahihisho. Siyo dhambi ya kusamehewa.

Hapendi mtu yeyote apotee

Tunaambiwa katika Rumi. 6:23 kuwa mshahara wa dhambi ni mauti.

Dhambi zisizosamehewa zitasababisha nafsi zipotee motoni.

Kristo amealika watu wote waokolewe, anasema: Math. 11:28-30, "*Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo mizito, nami nitawapumzisha. jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira yangu ni laini na mzigo wangu ni mwepesi.*"

Hapendi mtu yeyote apotee,bali wabadili nia zao na watubu.

2 Ptr. 3:9, "*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.*"

Mwenye dhambi lazima atii injili ya Kristo ndiposa apate msamaha kwa ajili ya dhambi zake. 2 Wathes.1:7-10, "*Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu; watakaodhibiwa kwa maangamizi ya milele kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake; yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kustajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile, kwa sababu ushuhuda wetu ulisadikiwa kwenu.*"

Dhambi zisizo samehewa zitahukumu nafsi Siku ya Hukumu. Nafsi nyingi ambazo hazija samehewa zita chukua muda wao katika jehanamu kwa sababu ya kutokuamini, kutokutii, na ugumu wa moyo.

Hitimisho

Je dhambi zako zimesamehewa au hazijasamehewa?

Bila kujali dhambi yako ni ya aina gani, Kristo alikufa kwa ajili yako.

1 Wakor. 15:3, "*Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi, mwenyewe ya kuwa Kristo alikuwa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko;"*

Msamaha siyo kazi rahisi. Iligharimu uhai wa mwana wa Mungu. Bila dhabihu hii na kuwekwa wakifu kwa damu yake hakutakuwa na msamaha. Lakini Bwana ataweza kusamehe tu kama tukitafuta msamaha wake kupitia imani na kutii mapenzi ya Mungu. Luka 6:46, *"kwa nini mnaniita, Bwana Bwana na hamfanyi nisemayo."*

Je dhambi zako zimesamehewa au bado hazijasamehewa? Usisubiri mpaka ukachelewa. Dhambi isiyosamehewa katika Hukumu inamaanisha kwamba mtu anapotea milele!

Yafuatayo ni hatua muhimu kwakufanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb.11:6, "Nilipokuwa katika shule ya sekondari (nilikuwa na miaka saba), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akaniambia kuwa alikuwa hamuamini Mungu. Kwa sababu nilikuwa nime batizwa, nilichukuwa nafasi ya kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ni mzuri, lakini hakuwa na hakika kwamba alimwamini Mungu. Lakini kuwa katika sehemu salama, labda angeweza kwenda kanisani, na akifa akasimama mbele ya Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri kwamba Mungu anaweza kumruhusu kuingia Mbinguni (kama kuna Mungu), na siyo katika moto (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima umuamini kwa moyo wako wote lasivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matendo. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* Matend. 11:18, *"... Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima .</u>* wakati ulipokuwa unalala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na ukafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani ya nyumba!" kwa hiyo ukachukua simu ya mkononi, na kwa haraka ukawapigia polisi, ukiwambia kuna mwizi ndani kwako, na ukawapa namba ya nyumba yako. Muda mfupi ukasikia wanafika na wanamashika mwizi. Mwizi akapiga kelele, "samahani; anaomba msamaha juu ya nini? Anaomba msamaha kwa sababu ameshikwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndiyo toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Hiyo ndiyo tunatakiwa tufanye kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Rumi. 10:9-10, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana <u>kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hatakupata wokovu."</u>* Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu imani (Kuamini), kutubu na kukiri ni "**KATIKA"** haki, maisha, au

wokovu. “Katika” inamaanisha kuelekea kitu Fulani; siyo kwamba mtu ameshapata.

- **Batizwa.** Ni katika ubatizo tu ambapo haki, maisha, na wokovu unapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa kutimiza haki yote, *“Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwakuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zika mfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninaye pendezwa naye.”* Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo zuri kufanya. Unaona ni jinsi gani ilimpendeza Mungu baada ya Yesu kubatizwa? Yesu pia akasema *“imekuwa **kwetu** kuitimiza haki yote.”* Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yote, si kwa sababu ni kwa ajili ya haki yetu.

  Kwa kweli, tusipobatizwa, bado tupo katika dhambi. “*Petro akawambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”* (Matend 2:38). Petro, umesema ubatizo ni kwa ajili ya nini? *“kwa ajili ya ondoleo la dhambi”.* Kwa nini watu wanaacha hatua inayotuondoa dhambi?

  Yesu aliamuru kuwa ili tuufikie wokovu ni lazima tubatizwe. *“Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.”* (Marko 16:15-16).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu hicho icho, “*Sasa unakawilia nini? Simama, na ubatizwe na uoshwe dhambi zako, huku ukiliitia jina la Bwana.”* (Matnd. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

  Ubatizo unaitwa maziko. “*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.”* Utuwetu wa kale lazima ufe ndani yetu. *“Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye ili mwili wa*

dhambi ubatilike tusitumikie dhambi tena." (Rumi. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumika katika damu ya Yesu Kristo ndani ya maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapo batizwa.

Hii hai maanishi "kunyunyiza. Andiko hilo juu inasema ubatizo ni maziko. Hatu peleki maiti makaburini na kuweka udongo kidogo juu yake; tunazika mwili.

Kama hujawa mkristo, kwa nini usifanyike leo?